OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI NYANG'ORO,
S.L.P. 1576,
IRINGA.
SIMU: 0768 007 121 / 0789 459 260

KUMB. Na. NYASS/ ADMISS/ 02/ 06 18.12.2020

JINA LA MWANAFUNZI:…….

SHULE YA MSINGI:……

S. L. P:……..

IRINGA

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYANG'ORO WILAYA YA IRINGA MKOA WA IRINGA MWAKA 2021

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Nyang'oro mwaka 2021. Hongera sana!

Ninaamini unatambua umuhimu wa elimu kwa maendeleo yako, familia yako, jamii yako na taifa kwa ujumla.

Shule ina mihula miwili kila mwaka kama ifuatavyo:-

i. Muhula wa I: unaanza tarehe 11.01.2021 hadi tarehe hadi tarehe 04.06.2021

ii. Muhula wa II: unaanza tarehe 05.07.2021 hadi tarehe 10.12.2021

Shule itafunguliwa jumatatu tarehe 11.01.2021 saa 1:30 asubuhi. Unatakiwa kuripoti siku hiyo tayari kwa kuanza muhula wa kwanza wa masomo. Karibu sana Nyang'oro Sekondari.

2. HISTORIA YA SHULE

Shule hii ni ya wananchi na ni ya kutwa. Inamilikiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Ilianza rasmi tarehe 18.04.2012. Shule imesajiliwa kwa namba S.4614 mnamo tarehe 30.04.2012. Shule ipo katika kijiji cha Nyang'oro, kata ya Nyang'oro, tarafa ya Ismani, Wilaya ya Iringa katika mkoa wa Iringa.

Shule ipo umbali wa takribani kilometa 50 toka Iringa mjini yalipo Makao makuu ya wilaya ya Iringa, na pia umbali wa takribani kilometa 4 toka kituo cha mabasi katika kijiji cha Nyang'oro, upande wa Magharibi mwa barabara kuu ya Iringa- Dodoma.

3. MAMBO MUHUMU YA KUZINGATIA

Yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia unapojiandaa kuja shuleni na wakati wote utakapokuwa mwanafunzi wa shule hii.

3.1: Sare ya Shule

a) Wasichana

i. Sketi mbili rangi ya khaki (**khaki na. 1).** Mshono wa **rinda boksi.**

ii. Blauzi nyeupe mbili za mikono mifupi.

iii. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba jozi mbili.

iv. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili.

v. Sweta langi ya damu ya mzee lenye shingo ya V (siyo nyekundu).

vi. Mavazi ya michezo (t- shirt, bukta, skin tight na raba).

vii. Waislamu wanaruhusiwa kushona Hijab sawa na rangi ya sketi na blauzi.

b) Wavulana

i. Suruali mbili rangi ya khaki (**khaki na. 1).** Mshono wa suruali **lazima uwe na marinda manne na itavaliwa kiunoni.**

ii. Shati nyeupe mbili za mikono mifupi.

iii. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba jozi mbili.

iv. Mkanda mweusi wenye upana usiozidi inchi 1½

v. Sweta langi ya damu yam zee lenye shingo ya V (siyo rangi nyekundu).

vi. Mavazi ya michezo (t-shirt, bukta, viatu vya michezo).

3.2: <u>Mahitaji ya Kitaaluma na Kibinadamu.</u>

a. Kitaaluma.

i. Daftari kubwa (counter books 2 quire) kumi.

ii. Peni, kalamu ya mkaa, mkebe, rula, ufuto na kichongeo.

iii. Kamusi ndogo ya kiingereza. (**ni muhimu sana kwa kidato cha kwanza).**

iv. Bunda moja la karatasi nyeupe au Rim (**atakabidhi ofisini anaposajiliwa na ni muhimu sana).**

b. Kibinadamu

i. Kadi ya huduma za matibabu- CHF au Bima ya Afya.

ii. Daftari dogo la matibabu.

iii. Pesa taslimu ya matumizi.

3.3: <u>Vifaa vya Usafi wa Mazingira, Usafi wa Mwili na Chakula.</u>

A. Wasichana waje na doo ya lita kumi moja, kwanja moja na mfagio wa chelewa mmoja.

B. Wavulana waje na jembe moja lenye mpini na mfagio wa chelewa mmoja.

C. Wasichana wataokaa hosteli waje na:

   i. Sanduku la chuma la kuwekea vifaa (trunker), "squeezer" ya kukaushia maji, "mopper" ya kudekia, khanga au kitenge, kandambili, sabuni, dawa ya meno, mswaki, kikombe, bakuli, sahani, kijiko, taulo za kike (pedi) na vifaa vingine muhimu.

   ii. Gauni la kushindia (shamba dress) la kitambaa cha rangi ya bluu **namba moja,** mshono wa solo refu chini ya magoti; na pia "truck suit" ya rangi ya bluu.

NB: mwanafunzi hata ruhusiwa kuvaa nguo za aina nyingine muda wote awapo katika mazingira ya hosteli isipokuwa kwa zile zilizoainishwa hapo juu.

4. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Pamoja na sheria hizi, shule imezingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi yenye dhamana ya elimu pia Ofisi Ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unapaswa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:-

i. Hesima iwe kwa watu wote; walimu, wafanyakazi wasio walimu, viongozi, wazazi, walezi, wanafunzi wenzako, jamii yote, wakubwa na wadogo.

ii. Ni lazima kuhudhuria vipindi vyote darasani kwa mujibu wa ratiba. Ikiwa mwanafunzi anaumwa, mzazi au mlezi wake alete taarifa

shuleni, **kamwe mwanafunzi haruhusiwi kumuombea ruhusa mwanafunzi mwenzie.**

iii. Ni lazima kushiriki kazi zote za nje na pia michezo.

iv. Hairuhusiwi kutoroka shule au kuacha shule. Mwanafunzi atatakiwa kuanza kidato cha kwanza na kuhitimu kidato cha nne.

v. Hairuhusiwi kutumia lugha ya matusi na dharau.

vi. Hairuhisiwi **KABISA** kwa mwanafunzi kuwa na simu ya kiganjani shuleni au nje ya shule. Ikiwa mwanafunzi anataka kuwasiliana na mzazi au mlezi wake amuone mwalimu husika apewe simu iliyoandaliwa na uongozi wa shule.

vii. Hairuhusiwi **KUTEMBELEA** maeneo yanaouza pombe, nyumba za kulala wageni na nyumba za starehe. Pia wanafunzi wote **HAIRUHUSIWI** kuwa mitaani (stand) kuanzia saa 12 kamili jioni.

viii. Ulevi wa aina yoyote hauruhusiwi kwa wanafunzi.

ix. Ni lazima kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule kwa wakati wote.

x. Ni lazima kuvaa sare ya shule wakati wote utakapotakiwa kufanya hivyo.

xi. Ni lazima kufahamu na kuheshimu mipaka ya shule na kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa masomo.

xii. Ni lazima kutunza mali za umma kama vile majengo, vitabu, viti, madawati, milango, vioo vya madirisha, n.k

5. <u>MAKOSA YANAYOWEZA SABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA MASOMO.</u>

i) Utoro wa siku tisini (90) mfululizo.

ii) Wizi.

iii) Uasherati na Ushoga.

iv) Ubakaji

v) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, ugoro n.k

vi) Kupiga au kupigana.

vii) Kuoa au kuolewa.

viii) Kupata au kusababisha mimba.

ix) Kutoa mimba.

x) Kuharibu, kuchafua au kudharau Bendera ya Taifa.

xi) Kuharibu mali ya umma.

xii) Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki kuvunja Amani na usalama wa shule na watu.

xiii) Kukataa adhabu kwa makusudi.

xiv) Kushtakiwa mahakamani ama kuhukumiwa kifungo.

xv) Kuwa na simu ya mkononi.

6. MAMBO MENGINE YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI.

i. Fomu ya afya ya mwanafunzi (Medical Examination Form) itakayojazwa na Mganga Mkuu wa Hopsitali ya serikali baada ya kumfanyia uchunguzi wa afya mwanafunzi.

ii. Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule hivyo kuahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

iii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi.

HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI NYANG'ORO

(sehemu ya kwanza ya fomu hii ijazwe na mwanafunzi na sehemu ya pili ijazwe na mzazi au mlezi).

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA

SEHEMU YA KWANZA

(Sehemu hii ijazwe na Mwanafunzi mwenyewe)

Mmi…… (Mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi niliyopewa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Nyang'oro. Aidha naahidi kutoshiriki migomo, fujo na kutotenda makosa ya jinai. Pia nitatia bidii katika masomo na kazi za shule nikitambua kwamba elimu nitakayopata ni kwa faida yangu, jamii na Taifa langu

Jina la Mwanafunzi:……

Sahihi ya Mwanafunzi:…….

Tarehe:……

SEHEMU YA PILI

(Sehemu hii ijazwe na Mzazi/ Mlezi)

Mimi…… (Mzazi/ mlezi) wa……. Nakubali/ sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda **WOTE** awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa walimu, viongozi na jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote za shule. Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote hadi atakapohitimu shule nikitambua kwamba elimu atakayopata ni kwa faida yake, jamii na Taifa kwa ujumla.

Jina la Mzazi/ Mlezi:…….

Sahihi ya Mzazi/ Mlezi:…….

Nambari ya simu:……

Tarehe:……

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS

NYANG'ORO SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be filled by Medical Officer in respect of all new students)

Full name:…….

Age:……..

1. Blood count (red and white):……
2. Urine examination:……
3. Stool examination:……
4. Syphilis:……
5. T. B test:……
6. Ear test:……..
7. Eye test:……
8. Spleen:……
9. Abdomen:……..
10. HIV/ AIDS:……..
11. Additional information or any other Physical, Mental, Hereditary or infectious diseases:…….....

Treatment after examination:……
…….

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above concerned student has been examined and found fit to pursue further education.

Signature:……

Designation:……

Station:……

Official stamp:……

Date:……

NB: Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali inayotambulika na serikali